

**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA RUKWA MHESHIMIWA
MAGALULA SAIDI MAGALULA ALIYOITOA KATIKA MKUTANO
MKUTANO MKUU WA JUKWAA LA WAKULIMA WA NGANO
MKOA WA RUKWA ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA RDC
TAREHE 23/09/2015**

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Jukwaa,
Katibu Tawala wa Mkoa,
Mkurugenzi wa utafiti wa Kanda,
Wakarugenzi wa Halmashauri za Wilaya,
Watafiti na Maofisa Kilimo,
Wakulima wangano,
Wadau wa zao la ngano,
Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote napenda kwa namna ya pekee kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuweza kuwasafirisha salama nyote mnaotoka nje ya Manispaa yetu ya Sumbawanga. "Karibuni Sana"

Aidha, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Viongozi wa JUKWAA LA WAKULIMA WA NGANO" kwa kunipa heshima hii ya kuwa mgeni rasmi katika mkutano huu muhimu ambao tutapata fursa ya kujadiliana namna ya kusonga mbele katika shughuli zetu za Kilimo cha zao hili la biashara la Ngano.

Hotuba yangu haitatofautiana na maelekezo niliyotoa jana wakati wa shughuli ya makabidhiano ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Sisi Mkoa wa Rukwa tunayo fursa nzuri ya kilimo kwa kuwa na mvua za kutosha na ardhi nzuri ya kilimo. Lakini hatujawekeza kiasi chakutosha ili kuwafanya Wakulima wetu kulima kwa "Tija" japokuwa tunapata mazao lakini kiwango cha mavuno hakilingani na nguvu kazi na eneo linalotumika kwa kilimo.

Jana nilimuuliza Afisa Kilimo namna tunavyofanya Kilimo chetu akanithibitishia kuwa Tija ni ndogo.

Nimetoa maelekezo ambayo ninarudia katika Kikao hiki.

(i)Wataalamu wetu wa Kilimo wanawajibu wa kuhakikisha Kilimo chetu kinafanyika kwa Tija. Nguvu kazi na Mavuno yatakayopatikana yalingane na eneo linalotumika kwa shughuli za kilimo

(ii) Usimamizi na Matumizi ya pemebejeo uwe wa uhakika

(iii) Halmashauri zishiriki katika kuweka mazingira wezeshi ya Kilimo cha ngano kwa kuongeza Tija ili zinufaike na mapato yatokanayo na zao hilo la biashara.

Mkoa na Halmashauri zinawajibu wa kuhakikisha Kilimo chenye Tija ni kipaumbele katika Mkoa wetu kwa kuwa kupitia kilimo chenye tija Wananchi wa Mkoa wetu watajiletea Maendeleo kwa kuongeza kipato.

Mkutano huu utoe maazimio na muda wa utekelezaji wake ili baada ya mwaka mmoja tufanye tathmini hatua tuliyopiga ya kufanya kilimo cha ngano chenye tija ndani ya Mkoa.

Ninawaomba Wataalamu kutoka Tasisi ya Utafiti wa Kilimo Uyole watusaidie katika kufikia malengo yetu hayo ya kilimo chenye Tija kwa tafiti mbalimbali ambazo zinaendelea kufanywa na taasisi hiyo.

Nimeelezwa kuwa madhumuni mahususi ya Mkutano huu ni kutathimini shughuli za jukwaa zilizofanyika mwaka uliopita na kupanga mikakati ya utekelezaji wa shughuli za jukwaa kwa mwaka ujao. Ni matumaini yangu kuwa kwa kukutana pamoja kutasaidia kuainisha mikakati thabiti itakayosaidia kuboresha shughuli za kilimo cha ngano ikiwemo upatikanaji wa pembejeo za kilimo, zana za kilimo, huduma za utafiti na ugani zitakazoweza ongezeko la uzalishaji, upatikanaji wa Chakula na masoko ya zao la ngano.

Ni matumaini yangu kuwa jukwaa hili litajikita katika kuhakikisha kuwa wakulima wa ngano wanatumia pembejeo za kilimo na kutekeleza maelekezo ya wataalam wa kilimo juu ya kanuni bora za kilimo ili kuongeza tija katika uzalishaji wa ngano.

Bila zana bora za kilimo wakulima wetu hawataweza kufikia malengo ya kuongeza uzalishaji wa zao la ngano. Ni matumaini yangu kuwa jukwaa hili litakuwa chachu ya upatikanaji wa zana bora za kilimo kama vile matrekta ya kulimia na mashine za kuvunia ngano.

Napenda kutoa wito kwa wadau wote wa zao la ngano walioshirikishwa katika jukwaa hili kushiriki kikamilifu katika kutekeleza wajibu wao kama

ulioanishwa katika katiba ambayo mtasajili hivi karibuni, ni vema Jukwaa hili likasajiliwa ili muweze kunufaika na masuala mbalimbali ambayo yatahitajika kisheria .

Kilimo kinahitaji uwekezaji mkubwa sana hivyo natoa wito kwa taasisi za fedha kuwaunga mkono wanajukwaa kwa kutoa mikopo yenye riba nafuu na ambayo ni rafiki kwa wakulima ili waweze kuzalisha zaidi ka kuyafikia masoko ya zao la ngano.

Nihitimishe kwa kuwashukuru tena kwa kunialika katika Mkutano huu muhimu wa jukwaa la wakulima wa ngano la Mkoa wa Rukwa. Mkutano huu uwe mwanzo wa kuwa na utaratibu endelevu wa kukutana kila Mwaka ili kutathmini mafanikio ya utekelezaji wa mambo mliojipangia na kupanga mipango ya kukabiliana na changamoto zitakazokuwa zimejitokeza.

Nawatakieni nyote majadiliano mazuri na michango itakayotuwezesha kufanya kazi pamoja na kwa ufanisi zaidi ili tufikie malengo ya kuwa na Chakula cha kutosha na kuchangia katika Uchumi na kuondoa umaskini ndani ya miaka mitano.

Baada ya maelezo hayo mafupi napenda kutamka kuwa mkutano umefunguliwa rasmi.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

Magalula S. Magalula

MKUU WA MKOA

RUKWA